# SULUBU BIN NGUVUMALI, MHUSIKA KATIKA *NYOTA YA REHEMA*: KIGEZO BORA KWA MTANZANIA WA TANZANIA YA VIWANDA

*Masoud Nassor Mohammed*
*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar -Tanzania*
*almanamo@yahoo.com*

## Ikisiri

*Fasihi ni taaluma muhimu katika maisha ya binadamu wa zama zote. Taaluma hii humfuata mwanadamu kadiri ya mapito yake ya kimaisha yanavyokwenda. Ni mwiko taaluma ya fasihi kupitwa na wakati. Tanzania ikiwa katika mkakati wa kufufua na kuimarisha viwanda, fasihi ina mchango mkubwa katika azma hiyo njema kwa maendeleo ya Watanzania wote, wa vizazi vyote. Mchango wa fasihi ya Kiswahili katika maendeleo ya viwanda haupo katika mahitaji ya viwanda vya uchapishaji wa kazi za fasihi tu, haupo kwa viwanda kuwasaidia na kuwahamasisha waandishi wa kazi za kubuni za kifasihi kupata fursa ya kuchapisha kazi zao tu, bali pia kwa namna ya pekee kuchota mifano bora ya kuiga kutokana na baadhi ya wahusika wa kazi za fasihi ambao waandishi wetu wamewahi kuwasawiri katika sanaa zao. Makala hii inanuia kumuangazia mhusika mmojawapo wa kifasihi katika riwaya ya Nyota ya Rehema kama mfano sadifu wa kuigwa na kila Mtanzania katika wakati huu nchi ya Tanzania inapoimarisha viwanda. Mbinu ya uchanganuzi matini imetumika kuibua matendo mfano yatokayo ndani ya uhusika wa Sulubu katika riwaya ya Nyota ya Rehema iliyoandikwa na Mohamed Suleiman mwaka (1972). Makala imeonesha kwa uwazi namna mhusika Sulubu alivyokuwa mstari wa mbele katika mambo mablimbali: kupambana dhidi ya wanaokwamisha maendeleo, kutoa elimu sahihi ya kilimo, kufahamu hali ya soko na mahitaji yake, kujikita katika ufugaji, kufanya kazi kwa bidii bila kukata tamaa pamoja na kuimarisha mashamba ambayo yalionekana hayafai kwa kilimo kama ambavyo Serikali ya Tanzania inavyofufua viwanda vilivyokufa kwa muda mrefu. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, makala hii ni muhimu kwa wananchi, wasomi na taifa la Tanzania kwa ujumla. Inaamsha ari ya Watanzania kufanya kazi kwa bidii ili kufufua na kuvilisha viwanda vya Tanzania malighafi zitokanazo na juhudi ya kazi zao wenyewe.*

*MASOUD NASSOR MOHAMMED - SULUBU BIN NGUVUMALI, MHUSIKA KATIKA NYOTA YA REHEMA: KIGEZO BORA KWA MTANZANIA WA TANZANIA YA VIWANDA*

## 1.0 Utangulizi

Dhana ya uchumi wa viwanda imekuwa ajenda muhimu hivi sasa nchini ya Tanzania. Tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani, aliyekuwa Rais wa awamu hiyo, hayati John Pombe Joseph Magufuli na Rais wa Awamu ya Sita Mhe. Samia Suluhu Hassan wamekuwa wakisisitiza azma ya Tanzania kujikomboa kiuchumi kwa kutumia viwanda. Bila shaka hii ni azma njema sana. Azma hii imeshaanza kutoa matunda kwani Shirika la Kimataifa linalohusiana na masuala ya uchumi duniani limeitangaza Tanzania kuingia uchumi wa kati. Nia ya kuukuza zaidi uchumi wa Tanzania isitegemee watu, taasisi au idara fulani pekee, bali ni jukumu la Watanzania wote kwa kutumia fani zote.

Kila mmoja ana jukumu la kuchangia kufikiwa kwa azma ya maendeleo endelevu ya Tanzania. Fasihi ya Kiswahili ni kipengele kimojawapo muhimu sana kinachoweza kuchangia kuimarisha uchumi wa viwanda kwa namna mbalimbali. Namna mojawapo ni kwa kuwaangalia wahusika wa kazi za fasihi namna wanavyoweza kutupa mafunzo bora ya kuwachochea Watanzania kujitegemea. Hivyo, makala hii imemtumia mhusika Sulubu wa riwaya ya *Nyota ya Rehema* kama kiigizo kwa Watanzainia wenye lengo jema na nchi yao.

## 2.0 Wasifu Mfupi wa Mwandishi wa *Nyota ya Rehema*

Katika mahojiano yake na Profesa Said Ahmed mwaka 1981, bwana Mohamed Suleiman amejitambulisha kuwa, ni mtu wa Koani Wilaya ya Kati - Mkoa wa Kusini Unguja. Amezaliwa mwaka 1943 na kukulia Koani mpaka katika umri wa miaka kumi na nne alipohamia mjini Unguja**.** Katika utafiti wake wa Shahada ya Umahiri Said (1981) ameeleza na kuifafanua sanaa ya Mohamed Suleiman kwa namna ya pekee. Ameeleza kuwa, kazi za Suleiman ni maarufu sana Afrika Mashariki. Watu wengi wanamuona kuwa mtu mwenye ujuzi mkubwa wa sanaa ya uandishi wa kazi za fasihi.

Said (ameshatajwa) ana maoni kuwa, Suleiman hawezi kufananishwa na mwandishi mwingine yeyote wa riwaya za Kiswahili. Kwake, huyu ni bingwa nambari moja katika tasnia ya uandishi wa riwaya. Anaona kuwa japokuwa anaandika masuala yanayofanana na waandishi wingine kimaudhui lakini Mohamed Suleiman amewapita wingine kwa matumizi ya lugha katika uandishi wake.

Anakiri mwenyewe Mohamed Suleiman kuwa, kuhamia kwake mjini kumepanua maarifa yake na utambuzi wa maisha. Aidha, kuanza na maisha ya shamba (kijijini) na baadaye ya mjini kumekuza kwa kiwango kikubwa uwezo wake wa lugha ya Kiswahili. Jambo hili limemfanya awe na uwezo mkubwa wa uteuzi wa maneno kutoka katika kamusi yake ya Kiswahili cha shamba na ile ya Kiswahili cha mjini chenye mchanganyiko wa maneno ya lugha na lahaja mbalimbali za Kiswahili. Angalia mfano ufuatao juu ya uwezo wa kilugha alionao:

> Rehema hakuona tabu kukosa kazi kwa Mansuri na Rozi, na kusema kweli alishukuru. Mapenzi aliyooneshwa na watu mbalimbali yaliuviza unyonge wake. Kuwaniwa kukamfunza majivuno. Sasa alikuwa akiitambua nafasi yake katika dunia hii. Alitanabahi kuwa umbo lake ni rasilimali yenye kutumainika. Maadamu mwanamume yeyote aliyepishana naye, akiwa topasi na ufagio wake au mtaalamu na kalamu yake, wote hawakuweza kujizuia wasigeuke kumtazama. Basi dunia haikukosa nafasi kwake. Palikuwa na vijana kemkem wa kitajiri walimuomba aishi pamoja nao, tayari kuzikidhi haja zake zote, alitembea nao na kufanya nao mahaba, na baadhi yao alikaribia kuwapenda. Walimchukua hotelini, vilabuni na michezoni ambako wenzake walikuwa wakikulilia, walimwambia wanampenda, akastaladhi na maneno yao. Walimsheheneza zawadi, akafaidika na ukarimu wao. Walimridhia aliyoyataka, akadeka na upole wao. Bali katika utajiri na tajiri wenyewe mlikuwa na kitu ambacho Rehema alikituhumu uovu. Walipomtajia kifungo pamoja nao, walimkumbusha idhilali ya marehemu mama yake, wao hawakuwa chochote zaidi ya baba yake aliyemkimbia. (uk:78)

Katika *Nyota ya Rehema* Mohamed Suleiman ameteua na kupanga vizuri lugha aitakayo kwa mujibu wa dhamira anayoikusudia na wahusika aliowabebesha dhamira hizo. Kuhusu usanii wake bwana Suleiman mwenyewe ameeleza kuwa, kuna wakati hukusudia kuiremba lugha na wakati mwengine huwa hakusudii kufanya hivyo, badala yake lugha yenyewe hujidhibiti katika matumizi yake. Hii inamaanisha kuwa, uwezo mkubwa wa lugha alionao, huwa unamuangazia moja kwa moja katika kuiremba lugha yake ya kifasihi kuonekana kama iliyopimwa kwa vipimo maalumu vya kisayansi ilihali ni vipimo vya kiuzoefu na weledi alionao.

Kwa upande wa usawiri wa wahusika, Suleiman ni bingwa wa kuwafanya wahusika wake waonekane watu halisi kabisa katika maisha. Angalia kwa mfano mhusika Sulubu na lafudhi aliyompa, mhusika Karim na lugha ya kilaghai aliyomsawiria, mhusika Mzee Pongwa na hekima za kiutuuzima

alizomsheheneza. Utauona ufundi na weledi wa mwandishi wa riwaya hii waziwazi kupitia wahusika hao.

**3.0 Wasemavyo Watafiti kuhusu Kazi za Mohamed Suleiman**

Mbatia (2016) ameandika juu ya mwandishi Mohamed Suleiman. Ameangazia zaidi riwaya zake mbili mashuhuri, *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976). Ameeleza kuwa, riwaya hizo zimezungumzia zaidi masuala ya kihistoria yanayohusu maisha ya Zanzibar. Amemtaja Mohamed Suleiman kuwa wa kwanza kuangazia masuala ya ukabaila, ukoloni na mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka (1964) pamoja na muungano wa Zanzibar na Tanganyika ulioasisiwa baada ya uhuru wa nchi hizo mbili. Mbatia (ameshatajwa) anaendelea kueleza kuwa, ingawa waandishi wengine waliandika pia juu ya masuala haya, kwa namna alivyomnukuu Bertoncini (1965), Mohamed Suleiman ndiye aliyeandika kwa kina na upevu juu ya masuala hayo. Amesema: "Mohamed Suleiman anatambulika nchini mwake kama mtunzi hodari zaidi wa riwaya ya Kiswahili" (tafsiri ya Mbatia, 2016). Mbatia anasisitiza kuwa, kama Kezilahabi alivyowakilisha kilele cha upevu wa riwaya Tanzania bara ndivyo Mohamed Suleiman alivyowakilisha kilele hicho visiwani Zanzibar.

> Mohamed Suleiman ni nguli wa uandishi wa riwaya. Ustadi wake kama mwanariwaya umetambuliwa na wengi. Kwa mfano riwaya yake ya kwanza, *Kiu* ilishinda katika mashindano ya uandishi yaliyoandaliwa na 'East African Publishing House' mwaka 1970 na Tunzo ya Kamati ya Kitaifa ya Kiswahili mwaka 1975. Riwaya yake ya pili, *Nyota ya Rehema* ilishinda tunzo ya fasihi ya Jomo Kenyatta. Mtindo wa riwaya hizi hasa ukwasi wa lugha yake iliyosheheni nahau na msamiati teule umetambuliwa na wahakiki kama vile Senkoro, Bertoncini, Said Ahmed na wengineo (Mbatia, 2016:244)

Naye, Khamis (1981) ametafiti juu ya ujumi katika riwaya za Mohamed Suleiman Mohamed. Amechunguza riwaya za *Kiu*, *Nyota ya Rehema* pamoja na hadithi zilizomo katika *Kicheko cha Ushindi*. Alibaini ufundi mkubwa wa kiusanii umejitokeza katika kazi za Mohamed Suleiman. Mtafiti mwengine aliyemgusia Suleiman ni Khamis (1998). Yeye

ameandika kuhusu matumizi ya elementi za kiisimu katika riwaya za Mohamed Suleiman. Katika makala yake anaeleza kuwa, mbinu zilizotumiwa na Mohamed Suleiman katika uandishi wa riwaya zake kwa kiasi kikubwa zimefanya kazi hizo zionekane na sura ya kishairi ndani ya nathari (*Poetic-Prose*). Kwa mujibu wa maelezo yake, Khamis (ameshatajwa) anafafanua kuwa, mbinu hizo zimefanikisha vizuri maudhui ya riwaya zenyewe. Riwaya alizozitumia katika uandishi wa makala yake ni *Kiu* na *Nyota ya Rehema*.

Mlacha (1984) yeye ametafiti dhamira katika riwaya za visiwani pamoja na mfanano wa wahusika wa riwaya hizo. Amechunguza riwaya zilizoandikwa baina ya miaka ya 1970 na 1980. Miongoni mwa riwaya alizozishughulikia ni *Nyota ya Rehema* inayohusika pia katika makala hii. Alibaini dhamira mbalimbali zilizoshughulikiwa na waandishi na kuziweka wazi kwa jamii. Mtafiti mwingine aliyezitazama kazi za Mohamed Suleiman ni Said (2015). Yeye amefanya utafiti juu ya matumizi ya ndoto katika riwaya za Kiswahili. Amechunguza dhana hiyo kwa kuzilinganisha riwaya za waandishi wawili; Mohamed Suleiman (*Kiu* na *Nyota ya Rehema*) na Said Ahmed (*Asali Chungu* na *Utengano*). Alidhihirisha kulingana na kuachana kwa matumizi ya ndoto katika riwaya hizo. Morava (1987) amechunguza mshikamano wa matukio katika riwaya za Kiswahili. Katika utafiti wake aliangalia riwaya ya *Kurwa na Doto* (Farsy,1960), *Adili na Nduguze* (Robert, 1966), *Duniani kuna Watu* (Abdullah, 1973) na *Nyota ya Rehema* (Suleiman, 1976). Ameonesha namna riwaya za Kiswahili zinavyojengwa kwa mshikamano wa matukio na jinsi matukio hayo yanavyofanikisha ujenzi wa maudhui na mtiririko wa kimasimulizi.

## 4.0 Muhtasari wa Riwaya ya *Nyota ya Rehema*

Riwaya ya *Nyota ya Rehema* ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka (1976). Imeandikwa na mwandishi mahiri wa Kizanzibari, ambaye pia ameandika riwaya nyingine mashuhuri ya Kiswahili iitwayo *Kiu*. Riwaya ya *Nyota ya Rehema* inazungumzia mambo mazito katika jamii ya Waswahili. Inamzungumzia Rehema mhusika mkuu wa riwaya hii. Rehema na nyota yake. Anazaliwa katika familia ya kitajiri yenye asili ya Kiarabu. Kwa jaala ya Mwenyezi Mungu, Rehema anazaliwa akiwa na rangi tofauti kabisa na rangi za wazazi wake. Si baba wala mama. Kuzaliwa na rangi tofauti na wazazi wake ndio unakuwa mwanzo wa kisa chake cha kusikitisha na kuhuzunisha katika maisha yake.

Hata hivyo, ilibainika baadaye kuwa, Rehema alifanana na bibi yake na kwamba hakupotea katika asili ya familia yake.

Baada ya kifo cha Aziza (mama wa Rehema), Rehema anachukuliwa katika kasri ya bibi Adila mke wa pili wa bwana Fuad. Anakabidhiwa mikononi mwa watumishi. Humo hakutumwa tu bali aliteswa pia. Hakudharauliwa tu lakini pia alibezwa. Hakunyanyaswa pekee lakini alifanyiwa kila aina ya ukatili kutoka kwa mabosi wake watumishi. Bosi wa watumishi wote (bibi Adila) naye alikuwa na yake ya kumfanyia Rehema. Cheo cha Rehema katika nyumba hii ni mtumishi wa watumishi.

Hakuwa na uhuru wa namna yoyote. Hakuangaliwa wala kutunzwa kwa vyovyote. Hakuulizwa shida yake wala mahitaji yake, bali alitumwa na kuonewa kwa namna zote walizotaka. Kwa muda wote alioishi humo alinyanyasika na kugugumia maumivu yaliyotokana na mateso waliyompa.

Fikra za ukombozi zinamwingia Rehema kupitia ndoto yake. Hapo anaamua kutoroka kuelekea kusikojulikana. Anaangukia mikononi mwa Sulubu. Sulubu anaishi pekee katika kibanda kilichotenganishwa na nyumba ya jirani yeyote yule. Anamfanyia aliyomfanyia bila ya ridhaa yake ilihali Rehema hajitambui. Baadaye anaelekea mjini ambako anakutana na Kidawa na kuanza kuishi maisha ya mjini katika kijumba chenye tafrani za mchana na usiku.

Akiwa hapo anapata kazi ya ulezi wa mtoto kwa Mansuri, mume wa Rozi. Hapo nyota yake inakumbwa na msukosuko mwingine mkubwa. Mansuri anauacha ubinadamu na kujivalisha uhayawani, anamtaka Rehema kimapenzi. Bi Rozi alipogundua, Rehema analazimika kukimbia na kutafuta kazi nyingine. Baada ya muda mrefu Rehema anatanabahi na kugundua utulivu wa Sulubu. Anaamua kumtafuta na kumuomba waishi pamoja. Wanashirikiana katika kufanya kazi za kilimo ndani ya majaribu kadhaa likiwemo lile la kunyang’anywa shamba lao.

Mwisho, mwandishi anamaliza kwa kuonesha kutokea mapinduzi yaliyosukumwa na kuhukumiwa kunyongwa kwa Sulubu baada ya kumuua Karim ambaye alikuwa ni mnyang’anyi na dhalimu mkubwa katika nchi hiyo.

### 4.1 Maudhui ya Jumla ya Riwaya ya *Nyota ya Rehema*

Riwaya hii kwa ujumla inazungumzia suala la ubaguzi wa rangi pamoja na uonevu na dhuluma za kitawala dhidi ya raia. Baadhi ya viongozi wa serikali wanaonekana kuhusika moja kwa moja katika kuwadhulumu wananchi mali zao kwa kutumia nguvu za kiutawala na udanganyifu wa kisheria. Karim mume wa Salma anajaribu kadiri anavyoweza kuhakikisha anajichukulia kila anachoweza kukipata kutoka kwa wanyonge.

Naye, Rehema anakataliwa na wazazi wake kwa sababu amezaliwa akiwa hafanani nao kwa rangi. Jambo hili linamkosesha haki yake ya msingi ya urithi na matunzo kutoka kwa baba yake. Mchanganyiko wa maonevu haya unaisukuma jamii kujikomboa kwa njia ya mapinduzi.

### 4.2 Wahusika katika *Nyota ya Rehema*

Riwaya ya *Nyota ya Rehema* imesukwa kwa wahusika mbalimbali kutimiza azma ya mwandishi kuyawasilisha maudhui yake. Waliojitokeza kubeba sehemu kubwa ya maudhui ya riwaya hii ni Rehema, Fuad, Sulubu na Karim. Wingine waliomo katika riwaya hii ni pamoja na Salma, Bikiza, Mzee Pongwa, Chiku, Kidawa, Ruzuna, Mansuri, Rozi na wingineo ambao wamebebeshwa dhamira mbalimbali kuijenga maudhui kuu ya *Nyota ya Rehema*.

#### 4.2.1 Mhusika Sulubu

Sulubu bin Nguvumali ni miongoni mwa wahusika wakuu watatu walioifanya riwaya ya *Nyota ya Rehema* ifane na isaniike barabara. Mrefu mweusi, mwembamba na mchapakazi asiyekata tamaa. Aidha, ni mkulima, mfugaji na mpenzi mkubwa wa burudani za uimbaji kwa kutumia marimba.

Makala hii hasa inalenga kumuangazia mhusika huyu na namna anavyoweza kutupatia mafunzo imara ya kuigwa na kila Mtanzania wa zama hizi za ufufuaji viwanda. Majukumu aliyopewa na Mohamed Suleiman, mwandishi wa riwaya ya *Nyota ya Rehema* kama kwamba yalitabiri ujio wa Hayati Rais wa Awamu ya Tano na Rais wa Awamu ya Sita wa Tanzania, kwa azma ya dhati ya kuchapa kazi na kupambana na kila kinachoashiria kuzuia azma hiyo.

Mhusika huyu kupitia matendo yake anatwambia vilevile tunavoambiwa hivi leo ‘asiyefanya kazi na asile’. Ameonesha kwa uwazi kuwa, maendeleo bila ya kufanya kazi hayataweza kufikiwa. Aidha, imebainika kila panapokuwa na nia ya dhati ya maendeleo katika jamii huwepo wapinzani wake ambao nao hufanya wawezavyo kuyakwamisha. Hata hivyo, Sulubu wa *Nyota ya Rehema* ni mfano bora kwa kila Mtanzania wa Tanzania ya viwanda katika kupambana na vikwazo vya aina yoyote ile katika safari ya kustawisha uchumi wa viwanda nchini Tanzania. Katika sehemu inayofuata tumechambua kwa mifano kutoka katika riwaya hiyo namna Watanzania wanavyoweza kunufaika na mhusika Sulubu kufikia azma ya kimaendeleo.

## 5.0 Vigezo Sadifu Kuelekea Tanzania ya Viwanda

Matendo mbalimbali yaliyooneshwa na bwana Sulubu yaliashiria uhodari, umakini, umadhubuti, na uchapakazi thabiti katika kujiletea maendeleo yake. Matendo hayo hapana shaka iwapo yatafuatwa na Watanzania wa Tanzania ya viwanda yanaweza kuwafikisha kirahisi katika uchumi wa viwanda kama serikali ya Tanzania ilivyopania. Yafuatayo ni baadhi ya matendo ya Sulubu ndani ya *Nyota ya Rehema* ambayo kwayo tunataraji yawe yenye kufaa kwa Watanzania wa leo**.**

### 5.1 Kumuua Simba kwa Kosa la Kula Kuku

Simba ni jina la mbwa wa Sulubu katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*. Sulubu alikuwa mpenzi mkubwa wa mbwa. Alimfuga na kumhudumia vizuri kwa chakula na usafi. Hakuwa mbali na mbwa wake wakati wote. Alikuwa rafiki na mlinzi wake wa karibu mno. Huzuni humwingia pale anapokuwa mbali naye. Pamoja na mapenzi hayo makubwa aliyompa, alipoanza tabia ya kula mifugo yake (kuku) mapenzi kwake aliyaondoa na kuamua kumtumbua mara moja kwa panga lake tena hadharani ili iwe fundisho kwa wingine. Mwandishi anaeleza:

> Hata siku ya tatu wakati Rehema alipokuwa akiwachungia bandani kuku wake wakati wa Magharibi alibaini kuwa kifaranga kimoja ambacho alikinunua kwa ajili ya mbegu kimepungua katika hesabu. Alimweleza Sulubu ambaye alikuwa uwanjani akitia tupa panga lake la kazi. Papo hapo hasira ilipanda katika uso wa Sulubu na sura yake ikabadilika,

> alinyanyuka kwa ghadhabu na akalenga panga lake sawa na simba aliyekuwa kalala uwanjani (uk:118)

Hiki kilikuwa kikwazo cha maendeleo ambacho Sulubu hakupenda kibakie. Alijitahidi kujiimarisha katika mifugo ili kunyanyua hali yake ya kiuchumi lakini mbwa alimkwamisha. Pamoja na mapenzi aliyokuwa nayo kwa mbwa huyo aliamua kumuondoa. Hakutaka awe na rafiki mkwamishaji wa maendeleo. Huu ni mfano dhahiri unaoakisi utendajikazi wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia awamu ya tano sio kwa kuua bali kuwaondoa mara moja katika nyadhifa walizoteuliwa wale wanaokwamisha katika malengo ya kiuchumi. Hata kama watu hao ni marafiki au jamaa wa karibu wa viongozi waliowateua. Serikali haiko tayari kumbakisha mtu yeyote katika nafasi ya uongozi ambaye anakwamisha juhudi za maendeleo. Ni kusema kwamba, hayati Rais Magufuli na mrithi wake Mhe. Samia Suluhu Hassan wanamsawiri vizuri mhusika Sulubu. Kama Sulubu alivyofanikisha ukombozi wa nchi katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* ndio matarajio ya Watanzania kwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anajipambanua kuwa, yeye na mtangulizi wake ni kitu kimoja. Watanzania wana matumaini ya ukombozi wa kiuchumi kutoka kwa Rais wao.

## 5.2 Sulubu Kumuua Karimu

Karimu alikuwa miongoni mwa viongozi wa serikali ambaye alitumia nafasi yake kuwanyang'anya wanyonge. Alikuwa mzoefu. Alikwishawaibia wengi sana katika raia wa nchi yake. Alimnyang'anya Rehema na Sulubu shamba lao la Ramwe. Waliponunua kishamba kingine huko Pakani, Karimu aliazimia nacho kukichukua kwa hila za kisheria. Hapo maji yalizidi unga kwa Sulubu. Hakuwa tayari tena kwa mara ya pili kurejeshwa nyuma kimaendeleo. Mwandishi anasimulia tukio lilivyokuwa:

> Aah! maskini alikuwa kishazoea kula mali za watu. Maradhi kama haya hayasikii dawa na kwa hivyo panga la Sulubu lililenga sawa na kiwiliwili cha mwivi! Shshap! Vipande viwili….!
> (uk:167)

Hiki kilikuwa kikwazo kingine cha maendeleo sio ya kina Rehema na Sulubu tu bali kwa jamii nzima. Sulubu alipokamatwa na kuhukumiwa kunyongwa kwa kosa la mauaji ya muuaji, jamii ilikuja juu na kwa kushirikiana na wanajeshi wazalendo yakafanyika mapinduzi yaliyoirejesha hadhi ya wanyonge katika nchi yao. Kinachosisitizwa hapa ni kwamba, kila Mtanzania awe mzalendo na mtamanifu wa maendeleo. Yanapokwamishwa na kikwazo chochote sheria ishike nafasi yake kuondoa kikwazo hicho. Huu ni mfano wa ujasiri na ukakamavu unaohitajika na kila Mtanzania mzalendo mwenye hamu ya maendeleo. Ingawa mwandishi amelionesha jambo hilo kwa sura inayotisha lakini kuna jambo muhimu la kujifunza. Tanzania ya leo ina sheria na taratibu za kudai na kutetea haki. Watanzania wanatakiwa kuwa jasiri kwa kufuata sheria zilizopo na si kuchukua maamuzi mazito nje ya vyombo vya sheria.

**5.3 Kutoa Elimu Juu ya Kilimo**

Sulubu akiwa mtaalamu na mzoefu wa mambo ya ukulima kwa siku nyingi, alikuwa tayari pia kumuelekeza Rehema naye awe na ujuzi wa mambo hayo. Huu ni moyo wa kizalendo, kuwa na ujuzi fulani na kuwapa wingine ili nao wanufaike na ujuzi huo. Hatimaye, kwa pamoja kila mtu aweze kuchangia maendeleo ya nchi na kujenga mustakabali wa uchumi imara. Angalia mfano huu:

> Sulubu alimfunza Rehema namna ya kupiga makoongo. Kupima baina ya koongo na koongo kwa mpini wa jembe. Kuatika. kupandikiza. kupalilia. kupanda na kuvuna na Rehema alionesha kuraghibika zaidi na konde kuliko jiko. (uk: 104)

Hapa mwandishi kupitia mhusika Sulubu anaeleza umuhimu wa elimu kwa jamii. Elimu ya kila jambo linalofanyiwa kazi. Katika wakati huu wa ufufuaji wa uchumi ni lazima elimu itangulie. Iwapo Watanzania hawatakuwa na elimu juu ya sekta wanazozifufua maendeleo hayataweza kupatikana. Sulubu ni darasa muhimu sana kwa Watanzania wote; raia na viongozi wao.

**5.4 Kufahamu Mahitaji ya Soko**

Jambo jingine ambalo ni mfano wa kuigwa kutoka kwa mhusika Sulubu ni umakini wake. Alikuwa anaelewa nyakati na mahitaji ya soko. Anajua

msimu upi alime nini na kwa kiwango gani. Jambo ambalo limefanya aweze kuuza mazao yake bila usumbufu wakati wote. Mwandishi anasema:

> Sasa Sulubu aliendelea kuisarifu ardhi yao kama alivyoona yeye mwenyewe ni bora. Alifika mbali na kufanya jitihada kubwa kusaka mbegu na mimea aliyoitaka na kuipanda alivyoona ndivyo kwa ujuzi wake wa miaka na miaka. Alikuwa akijua soko linahitaji tunda gani, wakati gani, na kwa kadiri gani. (uk:104)

Ni wazi kuwa wakulima wengi hukumbana na tatizo la masoko ya bidhaa zao wanazozizalisha. Hujikuta wamelima na wamevuna lakini mazao yao yanawaharibikia pasi na kuwa na soko la uhakika. Jambo hili hurejesha nyuma juhudi za wakulima. Sulubu hakuwa mjinga, alilifahamu vizuri soko lake na hivyo hakuharibikiwa na mazao yake. Watanzania wana mfano wa kuiga kutoka kwa Sulubu ili malighafi wanazozizalisha ziweze kuleta tija kwa taifa. Zisiharibike au kununuliwa na walanguzi kwa bei hafifu kwa kukosekana soko la uhakika.

## 5.5 Kufufua Shamba Pakani

Baada ya kunyang'anywa shamba la Ramwe, Sulubu na Rehema walinunua shamba Pakani. Hapakuwa na shamba kwa kweli lililokuwa likionekana lingefaa kwa kilimo. Hata hivyo, Sulubu alipashughulikia pahala hapo mpaka pakageuka rangi ya kijani. Pakavutia na pakaleta tija isiyotarajiwa. Mwandishi anasema:

> Sulubu hakuwa msemaji, hakuwa mwotaji, daima alikuwa yumo kazini au akijitayarisha kwa kazi. Mamluki wa kazi… hali ya mahali pale ilionesha kama kwamba hawakuwa na la kufanya isipokuwa kusubiri mauti. Tutashinda tu, Sulubu alisema huku akipapasa makali ya kisu chake... (uk:153-154)

Bila ya juhudi na kupambana hakuna mafanikio. Kuota pekee hakutoshi. Lazima mtu ajitume na afanye kazi kwa muda mrefu na kwa ujuzi. Namna Sulubu alivyofanya kuimarisha ardhi mpaka ikafaa kwa kilimo hakuna mtu angetarajia. Huu ni mfano mwema. Watanzania wanayo sababu ya kujifunza kwake. Mtu asiwe na ardhi akadai haina rutuba. Ipo namna ya kuirutubisha ardhi na ikafaa kwa kilimo. Kinachotakiwa ni juhudi na maarifa tu. Vipo viwanda vilivyotelekezwa kwa miaka mingi Tanzania vikidhaniwa kuwa havina tija. Ni wakati wa kuvifufua na kwa hakika ufufuaji umeanza. Matokeo chanya ya ufufuaji wa viwanda hivyo yanaonekana taratibu. Wakulima wazalishe malighafi kwa ajili ya viwanda hivyo ili kuwa na utoshelezano wa kiuchakataji.

**5.6 Ufugaji wa Kuku**

Sulubu hakuwa mfano katika kilimo cha mazao pekee. Alikuwa mfano pia katika ufugaji wa kuku na bata. Alijenga mabanda haraka na kumwachia Rehema atafute mbegu za kuku na bata ili kuanza ufugaji bila kuchelewa. Ufugaji nao uliwaitikia vyema na kuwapatia natija.

Alipomaliza kazi zake za kupalilia na kujaliza mimea katika sehemu ndogondogo zilizobaki, Sulubu alijenga mabanda ya kuku na bata. Naye, Rehema alianza kutafuta mbegu za mifugo kwa pesa alizopata katika mazao. Katika ukurasa wa 102, mwandishi anasawiri umeaji wa mifugo nyumbani kwa kina Sulubu.

Punde si punde nyumbani palihanikiza k-o-o-k-o-o za bata
na kwinyo kwinyo za kuku, mayai yakitafuta walaji…
(uk:102)

Uthubutu na ujasiri unahitajika sana kwa Watanzania katika zama hizi za ‘asiyefanya kazi na asile’. Kila mmoja lazima afikirie namna yake ya kufanya kazi na kunyanyua kipato chake na cha taifa kwa ujumla. Sulubu ameshatoa somo kupitia ujasiri na uthubutu wake katika matendo yake. Tanzania inapoelekea katika viwanda vya usindikaji nyama, ufugaji unapaswa kupewa kipaumbele.

**5.7 Kutokuwa Tayari Kuacha Kazi kwa Sababu Holela**

Alipokuwa kazini Sulubu mara zote alionekana kutokuwa tayari kupoteza muda kwa mambo yasiyo ya msingi. Aliinamia kazi yake na kutekeleza vizuri jukumu alilonalo. Alijua lengo lake. Alifahamu kwamba kufanya kazi kwa bidii ndiko kutakakomletea faida. Tunamuona Sulubu

alipofikiwa na Rehema kwa mara ya pili kwa lengo la kumtaka akaishi naye pamoja alimkuta anavunja nazi. Rehema alimwita mara mbili:

> Unasemaje pimdogo, Sulubu aliitikia bila kumtazama aliyemwita. Aliokota nazi iliyofuliwa na kuipiga dhoruba ya chuma kisha vipande vya nazi akavivurumishia juu ya chanja ya tanuri la moto (uk:94)

Hapa Sulubu anaonekana namna anavyojali kazi yake. Ni tofauti na baadhi ya watendaji na wafanyakazi katika jamii ya Tanzania ambao muda mdogo hufanya kazi na muda mrefu uliobakia ama hukaa tu bila kufanya kazi au huondoka kabisa katika eneo la kazi. Ni wakati sasa wa Watanzania kuiga utendaji kazi wa Sulubu ili kuufikia uchumi wa viwanda.

**5.8 Hitimisho**

Kazi za fasihi ni nguzo muhimu ya maendeleo ya nchi yoyote ile. Iwapo taifa litathamini na kuchota maarifa yasemwayo na waandishi wa fasihi kamwe taifa hilo halitabaki nyuma kimaendeleo. Wakati umefika kwa Watanzania wa kawaida pamoja na viongozi akiwemo Rais kuyatazama yaliyoandikwa na wanafasihi, kisha kuyafanyia kazi kwa namna inayofaa ili kuharakisha maendeleo ya taifa.

Imedhihirika wazi kupitia riwaya ya *Nyota ya Rehema* kuwa fasihi ina utajiri wa mali na elimu ndani yake. Hivyohivyo kwa kazi nyingine za kifasihi zinao mchango katika mustakabali wa maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla. Riwaya iliyodurusiwa katika makala hii na mhusika kigezo aliyechambuliwa matendo yake, amedhihirisha mchango wake wa kielimu, kimwamko na kimatendo kwa Watanzania. Watanzania waanzie hapo, wasonge mbele wajiletee maendeleo yao.

**Marejeleo**

Khamis, S.A.M. (1998). *Implication as a Literary Techniques in Mohamed S Mohamed's Novels Kiu and Nyota ya Rehema* in Rose-Marie Beck, Thomas Geider and Werner Graebna (eds). AAP Publishers.

Khamis, S.A.M. (1981). The Aesthentic Idioms of Mohamed Suleiman's Writings. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mbatiah, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili*: *Chimbuko na Maendeleo yake*. Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation.

Mlacha, S.A.K. (1984). Uhakiki na uchambuzi wa waandishi: Riwaya za visiwani 1970-1980 na ujenzi wa jamii mpya. *Mulika*. 16, 4-31.

Mohamed, M.S (1972). *Kiu*. Nairobi. Longhorn Publishers.

Mohamed, M.S (1976). *Nyota ya Rehema*. Nairobi. Oxford University Press.

Morava, E. C. (1987). Text cohesion and the sign: Connectedness between events in Swahili narrative. *Current Approaches to African Linguistics.* 4, 107-122.

Said, A. S (2015). Matumizi ya Ndoto katika Riwaya za Kiswahili: Ulinganishi wa Riwaya za Said Ahmed Mohamed na Mohamed Suleiman Mohamed. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.